




Alichokisema dada yake Vusi
Que va dire la sœur de Vusi ?



✎ Nina Orange
👤 Wiehan de Jager
📄 Matteo E. Mwita
🗣️ Kiswahili / French
|| Level 4

(imageless edition)

Storybooks Canada

storybookscanada.ca

Alichokisema dada yake Vusi / Que va dire
la sœur de Vusi ?


Written by: Nina Orange

Illustrated by: Wiehan de Jager

Translated by: (sw) Matteo E. Mwita, (fr) Isabelle

Duston, Veronique Biddau

This story originates from the African Storybook
(africanstorybook.org) and is brought to you by
Storybooks Canada in an effort to provide
children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons

[Attribution 3.0 International License.](https://creativecommons.org/licenses/by/3.0)

<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>






Siku moja asubuhi bibi yake Vusi alimwita na kumwambia, “Tafadhali peleka yai hili kwa wazazi wako. Wanataka kutengeneza keki kubwa kwa ajili ya harusi ya dada yako.”

...


Un matin de bonne heure, Vusi est appelé par sa grand-mère, « Vusi, s’il te plaît, peux tu amener cet œuf à tes parents. Ils veulent faire un gros gâteau pour le mariage de ta sœur ».



Alipokuwa njiani kuelekea kwa wazazi wake, Vusi akakutana na vijana wawili wanaokota matunda. Kijana mmoja akanyakua yai kutoka kwa Vusi na akalirusha kwenye mti. Yai likavunjika.

...

En allant chez ses parents, Vusi rencontra deux garçons en train de cueillir des fruits. Un des garçons s'empara de l'œuf de Vusi et le lança sur un arbre. L'œuf se cassa.



Dada yake Vusi alifikiria kwa muda, halafu akasema, "Kaka yangu Vusi, usijali zawadi, pia usijali keki! Tupo hapa pamoja, nina furaha. Nenda kavae nguo zako nadhifu na uje tusherehekee siku hii!"

...


La sœur de Vusi réfléchit un moment, puis elle a dit, « Vusi mon frère, les cadeaux me sont égaux. Je ne me soucie pas non plus du gâteau ! Nous sommes ici tous ensemble, je suis heureuse. Maintenant va mettre sur tes vêtements de fête et célébrons ce jour ! » Et c'est ce que fit Vusi.



“Umefanya nini?” Vusi akalia. “Yai lile lilikuwa kwa ajili ya keki. Keki ilikuwa kwa ajili ya harusi ya dada yangu. Dada yangu atasemaje kama hakutakuwa na keki ya harusi?”

...


« Qu’as-tu fait ? » cria Vusi. « Cet œuf était pour un gâteau, le gâteau du mariage de ma sœur. Que va dire ma sœur s’il n’y a pas de gâteau pour son mariage ? »



“Nifanye nini?” alilia Vusi. “Ng’ombe aliyekimbia alikuwa ni zawadi, ambayo nilipewa kama mbadala wa makuti niliyopewa na wajenzi. Wajenzi walinipa makuti kwa sababu walivunja fimbo niliyopewa na waangua matunda. Waangua matunda walinipa fimbo kwa sababu walivunja yai la keki. Keki ilikuwa kwa ajili ya harusi. Kwa hiyo hakuna yai, hakuna keki, na hakuna zawadi.”

...


« Que dois-je faire ? » s’écria Vusi. « La vache qui s’est enfuie était un cadeau, en échange du foin, que les constructeurs m’ont donné. Les constructeurs m’ont donné le foin, car ils ont cassé le bâton des cueilleurs de fruits. Les cueilleurs de fruits m’ont donné le bâton parce qu’ils ont cassé l’œuf pour le gâteau. Le gâteau était pour le mariage. Maintenant il n’y a pas d’œuf, pas de gâteau, et aucun cadeau ».



Vijana wale waliomba msamaha kwa kumchokoza Vusi. “Hatuna la kufanya kuhusu keki, lakini hii hapa ni fimbo kwa ajili ya dada yako,” mmoja alisema. Vusi akaendelea na safari yake.

...

Les garçons étaient désolés d’avoir taquiné Vusi. « Nous ne pouvons rien faire pour le gâteau, mais voilà un bâton de marche pour ta sœur, » dit l’un d’eux. Vusi poursuivit sa route.



Lakini wakati wa chakula cha jioni ng’ombe alikimbia kurudi kwa mkuilima. Na Vusi akapotea njiani. Akafika kwa kuchelewa sana kwenye harusi ya dada yake. Wageni walikuwa tayari wanakula.

...


Mais là l’heure du souper la vache s’échappa et retourna chez le fermier. Et Vusi se perdit en chemin. Il arriva très tard pour le mariage de sa sœur. Les invités mangeaient déjà.



Njiani alikutana na wanaume wawili wakijenga nyumba. “Tunaweza kutumia hiyo fimbo imara?” mmoja akaomba. Lakini fimbo haikuwa imara kwa kujengea, na ikavunjika.

...


En chemin, il rencontra deux hommes, qui construisaient une maison. « Pouvons-nous utiliser ce solide bâton ? » demanda l’un d’eux. Mais le bâton n’était pas assez solide pour la construction, et il s’est rompu.



Ng’ombe aliomba msamaha kwa kuwa mlafi. Mkulima alikubali kumpa Vusi ng’ombe aende naye kama zawadi kwa ajili ya dada yake. Vusi akaendelea na safari yake.

...

La vache était désolée d’avoir été si gourmande. Le fermier décida que la vache devait accompagner Vusi et être un cadeau pour sa sœur. Vusi poursuivit sa route.



"Mmetfanya nini?" Vusi akalia. "Fimbo hii ilikuwa zawadi kwa ajili ya dada yangu. Waangua matunda walimpa fimbo hiyo kwa sababu walivunja ya! la keki. Keki ilikuwa ni kwa ajili ya harus! ya dada yangu. Sasa hakuna ya!, hakuna keki, na hakuna zawadi. Dada yangu atasemaje?"

...

« Qu'avez-vous fait ? » s'écria Vusi. « Ce bâton était un cadeau pour ma sœur. Les cueilleurs de fruits m'ont donné le bâton parce qu'ils ont cassé l'œuf pour le gâteau. Le gâteau était pour le mariage de ma sœur. Maintenant il n'y a pas d'œuf, pas de gâteau, et aucun cadeau. Que va dire ma sœur ?



"Umetfanya nini?" Vusi akalia. "Makuti haya yalikuwa zawadi ya dada yangu. Wajenzi walimpa makuti kwa kuwa walivunja fimbo yangu niliyopewa na waangua matunda. Waangua matunda walimpa fimbo kwa kuwa walivunja ya! kwa ajili ya keki ya dada yangu. Keki ilikuwa kwa ajili ya harus! ya dada yangu. Sasa hakuna ya!, hakuna keki, na hakuna zawadi. Dada yangu atasemaje?"

...


« Qu'as-tu fait ? » s'écria Vusi. « Ce foin était un cadeau pour ma sœur. Les constructeurs m'ont donné du foin, car ils ont cassé le bâton des cueilleurs de fruits. Les cueilleurs de fruits m'ont donné le bâton parce qu'ils ont cassé l'œuf pour le gâteau de ma sœur. Le gâteau était pour le mariage de ma sœur. Maintenant il n'y a pas d'œuf, pas de gâteau, et aucun cadeau. Que va dire ma sœur ? »



Wajenzi waliomba msamaha kwa kuvunja fimbo.
“Hatuna la kufanya kuhusu keki, lakini tutakupa makuti umpelekee dada yako,” mmoja alisema. Na Vusi akaendelea na safari yake.

...

Les constructeurs étaient désolés d’avoir brisé le bâton.
« Nous ne pouvons rien faire pour le gâteau, mais voici du foin pour ta sœur, » dit l’un d’eux. Vusi continua sa route.



Njiani, Vusi akakutana na mkulima akiwa na ng’ombe.
“Una makuti mazuri, naweza kupata kidogo?” Ng’ombe akaomba. Lakini makuti yalikuwa matamu ng’ombe akayala yote!

...

Sur le chemin, Vusi rencontra un fermier et une vache. « Quel foin délicieux, est-ce que je peux en prendre un peu ? » demanda la vache. Mais le foin était si bon que la vache a tout mangé !